



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA
JIMBO LA TANDAHIMBA**

Kumb. Na.LA./121/220/03/54

Tarehe 21/09/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la TANDAHIMBA kwa kuzingatia kanuni ya 14 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Watendaji wa Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kama ifuatavyo:-

- 1. WASIMAMIZI WA VITUO VYA KUPIGIA KURA NAFASI - 491**
 - 2. WASIMAMIZI WASAIDIZI WA VITUO VYA KUPIGIA KURA NAFASI - 982**
 - 3. KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA NAFASI- 491**
- A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
 - (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
 - (c) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
 - (d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
 - (e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba.
- B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI ZA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
 - (b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;
 - (c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanyia kazi;

- (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
- (f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

C. MALIPO

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo:-

- i. Msimamizi wa Kituo siku ya Uchaguzi atalipwa posho ya Tzs. **35,000** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs **15,000** kwa siku moja na nauli Tzs **20,000**;
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Tzs. **30,000** kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs **15,000** na nauli Tzs **20,000**; na
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Tzs **30,000** kwa siku moja na posho ya chakula Tzs **15,000**.

D. MASHARITI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.

- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- Maombi yote yaambatane na Vyeti vya taaluma, nakala za Vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa kwa mujibu wa Tangazo hili.
- Waombaji waambatishe picha mbili 'Passport size' za hivi karibuni.
- Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Septemba , 2020.**

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni:-

Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Tandahimba
S. L. P 03
TANDAHIMBA

Said A.Msomoka

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA TANDAHIMBA**